# KUTOWAJIBIKA KATIKA UWEKEZAJI

AGRICA NI MFANO WA MRADI WA MAENDELEO ULIOHARIBIKA TANZANIA



## Shukrani

Timu ya watafiti kutoka Taasisi ya Oakland ikisaidiwa na utafiti, maandiko, dawati la mapitio ya maandiko, na utafiti wa ripoti hii chini ya usimamizi wa Anuradha Mittal kati ya 2011 na 2015, imewahusisha: Frédéric Mousseau, Arya Tajdin, Dylan Farrell-Bryan, Kevin Hull na Brittany Young.

Ripoti ya mwisho, iliyokusanya utafiti wa awali, iliandikwa na Mikael Bergius, mshiriki katika Taasisi ya Oakland, kwa msaada na usimamizi wa kihariri kutoka kwa Frédéric Mousseau na Anuradha Mittal

Tunatambua washiriki wote wa utafiti huu ambao walichangia katika ripoti hii, hasa wenyeji wanaozunguka mashamba ya KPL. Shukrani za dhati kwa Jumanne Abdallah kwa msaada wa utawala na Aisha Mshihiri kwa msaada wa utafiti. Tunapenda pia kumshukuru Carter Coleman, Mkurugenzi Mtendaji wa AGRICA, kwa kushirikiana katika taarifa na kujibu maswali yetu.

**Usanifu**: Amymade Graphic Design, amymade@gmail.com, amymade.com

**Mhariri nakala**: Elizabeth Fraser

**Picha ya jalada**: KPL kupanda na mashamba. © Greenpeace

**Tafsiri :** Kazi hii imetafsiriwa kutoka katika Kingereza kwenda kwenye Kiswahili na Maulid Mpamba

**Wachapaji**:

***Taasisi ya Oakland*** ni taasisi yenye sera huru yenye jumuiya ya washauri mabingwa wenye kuleta mawazo safi na hatua madhubuti zaidi za kijamii, kiuchumi, na masuala ya mazingira.

***Greenpeace Africa*** ni sehemuhuru ya shirika la kimataifa linaloendesha kampeni zinazojaribu kubadili mitazamo na tabia, ili kulinda na kuhifadhi mazingira na kuendeleza amani.

***Global Justice Now*** inahamasisha dunia ili rasilimali zidhibitiwe na wengi, si wachache, na kufanya kazi kwa mshikamano katika harakati za kupambana na dhuluma za kijamii.

Hati miliki © 2015 na Taasisi ya Oakland

Nakala zinaweza kutumika bila ya malipo kwa madhumuni ya utetezi, kampeni, elimu, na utafiti, kwa kuzingatia kuwa chanzo kinatambulika kikamilifu. Wamiliki wa hati miliki wanawataka watumiaji wote wasajiliwe kwanza kwa madhumuni ya kufanya tathmini. Kwa kuiga katika hali nyingine yoyote, kutumia tena katika machapisho mengine, au tafsiri au mabadiliko, ruhusa lazima itumike.

**Kwa taarifa zaidi**:

**The Oakland Institute**
info@oaklandinstitute.org
PO Box 18978
Oakland, CA 94619
Marekani
www.oaklandinstitute.org

**Greenpeace Africa**
info.africa@greenpeace.org
PostNet Suite 125, Private Bag X09
Melville, Johannesburg, 2109
Africa Kusini
www.greenpeace.org/africa

**Global Justice Now**
offleyroad@globaljustice.org.uk
66 Offley Road
London SW9 0LS
Uingereza
www.globaljustice.org.u

## Ufupisho


Mashamba ya kilombelo (KPL) yana ukubwa wa hekta 5,818 (ha) za mpunga zilizo katika kiini cha rutuba cha Bonde la Kilombero, Tanzania. Mbali na kuendeleza mashamba makubwa ya mpunga, KPL inafanya kazi na wakulima wadogo wadogo kupitia mashamba darasa yanayozingatia mfumo wa teknolojia ya ongezeko la mpunga (SRI) . Mradi wa uwekezaji unapata msaada mkubwa wa kifedha na kiufundi kutoka taasisi za maendeleo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Idara ya Kimataifa ya Maendeleo ya Uingereza (DfID) na USAID[1]. Ripoti hii inatoa matokeo ya uchunguzi uliofanywa Tanzania kati ya mwaka 2011 na 2015 ya mradi wa uwekezaji wa KPL, ukiangazia uzoefu unaopatikana katika jamii jirani.

Matokeo makuu ya ripoti hii ni kama yafuatayo: Kwanza, wakati KPL imecholwa kama mradi wa kweli kwa uwajibikaji na uwekezaji[2], wanakijiji katika jamii jirani wanalalamikia athari mbaya kwa maisha yao kutokana KPL kuchukua ardhi yao. Pamoja na kupitishwa kwa miongozo ya Benki ya Dunia juu ya makazi ya lazima iliyoahidi kuboresha, au angalau kurejesha maisha ya watu walioathiriwa na mradi, KPL ina kesi nyingi, inadaiwa kushindwa kulinda maslahi ya wanajamii ambayo yanaripotiwa kupotea. Fidia zinazotolewa kwa ajili ya hasara ya ardhi na nyumba inaonekana kuwa chini ya kiwango kwa kiasi kikubwa, haikuruhusu wakazi walioathirika kutokana na mradi kupata ardhi ya kutosha kwa maisha yao.

Pili, mpango wa mfumo wa teknolojia ya ongezeko la mpunga (SRI) wa mashamba ya kilombelo (KPL) ulianzishwa kama njia ya kushamirisha uzalishaji katika kitovu cha mashamba na kutoa fursa kwa wakulima wa ndani. Kwa utekelezaji wa teknolojia mpya, ripoti ya wakulima imeboresha mavuno ikionesha kupatikana kwa wingi ukilinganisha na kitovu cha mashamba ya kilombelo (KPL) katika suala la uzalishaji kwa hekta[3]. Pamoja na kuimarika kwa mavuno, wakulima wa ndani wanadai kuwa kuanzishwa kwa mpango huu kumewafanya wengi kukata tamaa. Wakikabiliana na ulipaji wa madeni, wakulima wanadai kulazimika kufanya mauzo ya mazao yao kwa dhiki. Matatizo hayo yanaonekana kuhusiana na mikataba iliyoanzishwa baina ya wakulima wadogo na KPL. Aidha, kwa mujibu wa wafanyakazi waliopita, ajira za mashamba zimeshindwa kuzalisha faida zinazoonekana kwa jamii kutokana na mishahara midogo na kukosa fursa za kupata ajira za kudumu.

Tatu, ripoti hii imewaondoa wasiwasi kuhusu madhara ya mazingira kutokana mradi huu katika maeneo ya mazingira na viumbehai vyenye thamani kubwa. Matumizi ya muda mrefu ya kemikali za kilimo yanaibua wasiwasi juu ya uwepo wa mazingira yao katika ardhi, maji na uchafuzi wa mito iliyokaribu nao, mikondo ya maji, na maeneo yenye unyevu unyevu yanayotumiwa na Wanakijiji wa jamii asilia[4]. Wanakijiji wanaozunguka mashamba ya kilombelo (KPL) wanadai kuwa na uzoefu wa madhara kadhaa kutokana matumizi ya madawa ya kilimo yanayofanywa na KPL ambayo ni kusababisha mmonyoko wa ardhi[5]. Aidha, mipango ya baadaye ya KPL ya kuutumia mto Mngeta kwajili ya umwagiliaji inatia mashaka katika mazingira ambapo kuna taarifa ndogo za kuaminika juu ya upatikanaji maji na mahitaji ya maji katika mazingira magumu ya mafuriko na watumiaji wa mito[6]. Wataalam wanadai kuwa Mto Mngeta tayari unakabiliwa na madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa[7].

Kwa kuhitimisha, ripoti hii inaeleza matatizo katika kujenga mahusiano ya manufaa na usawa kati ya maslahi ya wakulima wadogo na wale wa wakulima wa biashara kwa kiasi kikubwa. Inahoji jukumu la kilimo cha mashamba makubwa katika maendeleo ya kilimo kwasababu yanaleta matatizo zaidi kuliko kutatua, hata pale wanapojaribu kuwahusisha wakulima wadogo katika mikakati yao. Matokeo ya utafiti yaliyotolewa katika ripoti hii yanatoamashaka makubwa juu ya misaada mingi ya kifedha inayoelekezwa katika kusaidia mashirika yanayoongoza maendeleo ya kilimo. Hii ni mahususi hasa katika mazingira ya maendeleo ya kitanzania ambapo wakulima wa biashara kwa kiasi kikubwa wanamatarajioa makubwa zaidi.

# Utangulizi

Jukumu la kilimo katika kukuza maendeleo limekuwa likizidi kutambulika katika muongo uliopita. Si tu inakuchukuliwa kama njia kwa serikali na wafadhili kukabiliana na changamoto kubwa za uhaba wa chakula na umaskini, lakini imekuwa ni fursa nzuri kwa wawekezaji wa kilimo cha biashara ya kimataifa. Katika mazingira ya kutatua migogoro ya kimataifa katika chakula, fedha, nishati, na hali ya hewa, kumekuwepo na ongezeko katika miaka ya hivi karibuni katika uwekezaji wa kilimo kwa nchi zinazoendelea. Ardhi na Kilimo vimekuwa mikakati mipya ya mali kwa wawekezaji wa kitaifa na kimataifa mara nyingi wamekuwa wakifanya kazi pamoja na serikali, wafadhili, na taasisi za maendeleo ya kimataifa.

Uwekezaji wa moja kwa moja (FDI) katika kilimo kwa nchi zinazoendelea umetoa takribani mara mbili ya fedha za kimarekani kutoka wastani wa dolla 13 hadi kufikia dolla 25 za kimarekani kwa mwaka 2003 na 2008/09 na Afrika kuwa moja ya mpokeaji mkuu[8] . Wakati hatua hii ikipungua kasi tangu mwaka 2009, wimbi la uwekezaji wa kilimo bado ni kubwa. Watetezi wa mwelekeo huu wanapendekeza kwamba maendeleo ya kilimo cha viwanda kwa mtazamo mkubwa katika kuongeza mavuno si tu kuwa na faida kwa wawekezaji, vilevile ulete upatikanaji wa chakula na maendeleo kupitia fursa za ajira na miundombinu mipya, pamoja na kulinda mazingira[9]. Pamoja na ahadi hizo, utafiti unaonyesha kwamba jumuiya jirani zinazozunguka miradi ya uwekezaji zinategemea faida kuliko hasara. Upatikanaji mkubwa wa ardhi, mara nyingi umeboresha uwepo wa chakula, maisha, lakini kufanya haki ya ardhi vijijini kuwa mashakan
Ili kuondoa upinzani, wawekezaji wakubwa wa ardhi, pamoja na washirika wao katika serikali na taasisi za maendeleo, wanashirikiana kupiga porojo za kisiasa. Kwa kuwaunganisha wakulima katika mlolongo wa thamani wa kimataifa katika pembejeo na pato katika uzalishaji, inategemewa kwamba kupitia mpango wa ukuaji wa kilimo cha mkataba kwa kushikamana na mashamba makubwa ya asili, wakulima wadogowadogo watakuwa na fursa ya kupata teknolojia ya kisasa ambayo itaongeza tija na kipato [11]. Kuingizwa kwa mikakati hii kunahusishwa kama uwajibikaji wa kijamii katika uwekezaji kwa kuwathamini wazalishaji na pengine kuwaweka kando na soko la kimataifa[12].

Tanzania-imejaliwa kuwa na utajiri wa rasirimali za asili za kila aina na kuwepo kwa ardhi yenye rutuba ambayo haijawahi kutumika inadhaniwa kuwa ardhi ambayo bado haijatumika kwa uzalishaji wa chakula na ukuaji wa kiuchumi. Ni kwa sababu hii Tanzania inakuwa miongoni mwa nchi nyingi sana katika Afrika zinazolengwa na kilimo cha FDI[13].
Tanzania imefanya kilimo kuwa kipaumbele cha juu katika maendeleo yake kwa kupitia mpango wa Kilimo Kwanza (kilimo kwanza) uliopitishwa mwaka 2009. Mpango huu uliibuka ili kutambua umuhimu mkubwa wa kilimo kwa uchumi wa Tanzania. Yapata asilimia 75 ya jumla ya watu milioni 45 hujihusisha katika kilimo, wakikifanya kuwa uti wa mgongo muhimu wa uchumi wa Tanzania. Kwa kifupi, Kilimo Kwanza kinataka kuifanya biashara kuwa ya kisasa katika sekta ya kilimo na kuongeza tija kupitia ushirikiano wa umma na binafsi. Hii inalenga kuhamasisha sekta binafsi kwa kujenga motisha katika uchumi wa kitaifa na kimataifa kuingizwa katika sekta ya kilimo[14]. Lengo kuu la kilimo ni kufikia "Mapinduzi ya Kijani" kwa kukuza mahusiano, mafanikio ya kilimo cha biashara, yatakayowanufaisha wakulima wadogo wadogo wa Tanzania kupitia kuboresha upatikanaji wa chakula, kupunguza umaskini, na kuhakikisha mazingira endelevu[15].

Katika jitihada za kutekeleza Kilimo Kwanza, Rais Kikwete alizindua mpango kabambe mwezi Mei 2010 wenye ushirikiano baina ya sekta za umma na binafsi unaojulikana kama ***Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania*** (SAGCOT) (Box 1). Alielezea mpango huu kama jitihada kubwa za kilimo katika historia ya Tanzania[16]. Zikiwemo sehemu zenye rutuba ndani ya nchi, SAGCOT inalenga kutoa maendeleo yenye nguvu kwa kuunganisha wakulima wadogowadogo na viwanda vya huduma ya kilimo za kimataifa hasa kwa njia ya "kilimo cha asili na kwa kukua upesi "mipango itakayowezesha wakulima wadogo kupata pembejeo, vifaa, ongezeko la thamani na masoko kwa urahisi[17]. Mpango wa SAGCOT una nia ya kuweka" Kilimo Kwanza katika mwendelezo "[18].

Bonde la Kilombero-huchukuliwa kama chanzo cha "chakula" nchini Tanzania na ni moja ya maeneo muhimu yaliyolengwa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo chini ya mpango huo wa SAGCOT. Bonde hilo lenye rutuba tayari lina mashamba kadhaa ya asili yenye ukuaji wa haraka ambayo yote yalianzishwa kabla ya uzinduzi wa SAGCOT. Moja ya hayo ni ***Kilombero Plantations Ltd*** (KPL).

KPL ina hekta 5,818 zenye mashamba ya mpunga yaliyoko katika Bonde la Kilombero, linadhaniwa kuwa ni moja ya maeneo bora yanayofaa kwa ufugaji na kilimo cha mpunga katika Afrika Mashariki. Kwa

**SANDUKU 1: UKUAJI WA KILIMO UKANDA WA KUSINI (SAGCOT)**

SAGCOT ni mpango wa ushirikiano wa umma na binafsi kati ya Serikali ya Tanzania, kilimo cha mashirika, wafadhili, na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs). Lengo kuu ni kuinua wakulima wadogo kutoka kwenye umaskini, kuimarisha usalama wa chakula, na kukuza maendeleo ya kiuchumi wakati huo ukihifadhi mazingira. Uwekezaji wa SAGCOT unatoa mwongozo nakuonesha fursa na mikakati ya kipindi cha zaidi ya miaka 20 ijayo katika kufikia "Mapinduzi ya Kijani" nchini Tanzania. Umepanga kuzifanya hekta 350,000 za ardhi kuwa katika uzalishaji wa faida; kubadili wakulima wadogo 10,000 wawe katika kilimo cha biashara; kutengeneza fursa 420,000 za ajira mpya; kuinua watu milioni 2 kutoka katika umaskini; na kuzalisha dolla 1.2 bilioni katika mapato ya kilimo kila mwaka ifikapo mwaka 2030. SAGCOT imepanga kufanya ujenzi wa barabara, mabwawa, mifumo ya umwagiliaji, na upanuzi wa kilimo cha biashara. Ili kufanikisha hili, SAGCOT itaendelezwa katika maeneo yaliyowekwa ya kipaumbele yatakayoitwa cluster , ambayo yamekuwa yakitambuliwa kama sehemu zenye uwezo ambazo hazijatumika kwa ajili ya maendeleo ya kilimo. Cluster zimeunganishwa katika maeneo ya jirani yanayoshiriki nguzo za miundombinu pamoja, kama vile Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) mfumo na Bandari ya Dar es Salaam, kuwezesha mahusiano katika masoko ya kimataifa kwa ajili ya matokeo ya kilimo kama vile pembejeo. Maendeleo ya cluster kimsingi yanaendeshwa na sekta binafsi kwa kuzingatia fursa za kibiashara ambazo zipo katika kila eneo kwa lengo la kuvutia uwekezaji ili kuleta mahusiano katika vipengele vyote vya thamani katika kilimo. Eneo la bonde la Kilombero lenye nyumba za KPL- ni moja ya cluster sita ambazo zimekuwa zikitambulika.[22] Muungano mpya wa Usalama wa Chakula na Lishe bora wa Mataifa 8 Makubwa Duniani (G8) umechukua Mpango wa SAGCOT kama mfano wa kuigwa kwa maendeleo ya kilimo.

nyongeza katika kuendeleza mashamba makubwa, Mradi wa KPL umelenga kufanya kazi pamoja na wakulima wadogo wadogo kwa njia ya kuondoa mtindo msingi katika mfumo wa Teknolojia ya Ongezeko la Mpunga (SRI)[19]. Mpango wao wa biashara unashabihiana vizuri na malengo makuu ya mlolongo wa thamani ya ushirikiano asilia SAGCOT. Hii ndio sababu ya kwa nini KPL inaungwa mkono na serikali ya Tanzania, wahisani na taasisi za maendeleo kama mradi imara chini ya SAGCOT, na inasifika inayowajibika katika uwekezaji wa kilimo[20].

Pamoja na kuwa nyuma kiufasaha, ambayo inatoa mfano wa ukuzaji kwa sura ya uwajibikaji wa kijamii na uhalali, maswali muhimu yanaulizwa kuhusu madhara yake katika ardhi[21]. Ripoti hii inachunguza baadhi ya maswali haya kupitia uchambuzi wa mradi wa uwekezaji wa KPL, hasa kwa kuchunguza madhara yake katika jamii. Ripoti inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti uliofanyika nchini Tanzania katika vipindi kadhaa kati ya 2011 na 2014. Nia yetu ni kutoa sauti kwa jamii na kuwapatia jukwaa la kushiriki maoni yao kuhusu uwezo wa mashirika ya uwekezaji.

Ripoti inaendelea katika sehemu sita: Kwanza, inatoa historia juu ya mashamba ya KPL, muundo wake na mipango. Pili, inaangalia katika suala la ardhi na kujadili baadhi ya vipengele muhimu kuhusiana na uanzishwaji wa kiini cha mashamba ya KPL. Sehemu ya tatu inahusika na muungano wa sehemu za thamani ya kampuni kwa kutathmini madhara yake katika ukuaji. Sehemu ya nne inazungumzia fursa za ajira zinazotokana na KPL. Katika sehemu ya tano, masuala muhimu ya mazingira yanayohusiana na mradi yameibuliwa. Sehemu ya sita na ya mwisho ya ripoti inatoa maoni ya kuhitimisha na tafakari.



Mashamba ya mchele mashamba Agrica. © Greenpeace

## Kuhusu Ripoti

KPL ilianzishwa mwaka 2007 kama shirika la umma na binafsi kwa ushirikiano kati ya Agrica Tanzania Ltd (ATL) na Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA). ATL ni kampuni ndogo kabisa inayomilikiwa na Agrica Ltd, kampuni ya Uingereza iliyosajiliwa katika bandari ya kisiwa cha Guernsey. Agrica Ltd ilianzishwa mwaka 2005 kwa malengo ainishwa, "kuendeleza wakulima wa biashara endelevu barani Afrika[24]." Kwa kuimarisha usalama wa Afrika, malengo ainishwa ni kukuza ongezeko la mahitaji ya chakula kimataifa, kukua kwa masoko ya ndani katika bara la Afrika na kuongezeka kwa upatikanaji wa chakula duniani[25].Mpango wa biashara wa Agrica unaeleza:

> "Kupanda kwa mahitaji ya kimataifa kwa ajili ya chakula na malisho, pamoja na kushuka kwa tija na kutokuwa na uhakika wa usambazaji wa siku zijazo, kuwepo kwa nafasi za kuvutia za uwekezaji. [...] Ukuajia wa wa haraka masoko ya ndani Afrika unahitaji uboreshwaji wa kisasa, mashamba makubwa kwa ajili ya upatikanaji wa chakula cha ndani na nje ya Afrika[26]. "

Ikiwa kama sehemu ya mahusiano ya umma, RUBADA, ni wakala wa shirika la umma la kiserikali lililoanzishwa mwaka 1975. Misingi kazi yake ni pamoja na kukuza uwekezaji na uwezeshaji wa shughuli za maendeleo ndani ya eneo la ardhi katika maeneo yote ambayo mto Rufiji unatiririka[27].

Wanahisa wakuu wa Agrica ni kampuni ya Pasifiki Sequoia,Norfund (kampuni ya uwekezaji inayomilikiwa na serikali ya Norway) na Rasilimali Kilimo Afrika (African Agricultural Capital-AAC)[28] . Kampuni ya Pacific Sequoia ni sehemu ya *Capricorn Investment Group* (CIG), ambayo inasimamia mali za bilionea wa Canada na mfadhili Jeffrey Skoll kupitia mfuko wa Skoll (Skoll Foundation). Mfuko kwa sasa unamiliki takribani dolla za Kimarekami bilioni nne (4) kama jumla ya mtaji kupitia vyanzo mbalimbali katika, mfuko wa uwekezaji kimataifa na uwekezaji wa moja kwa moja[29]. Uwekezaji Capricon katika Agrica unafikia dolla za kimarekani milioni 17[30].

Lengo kuu la Norfund, mfuko wa uwekezaji wa Norway kwa nchi zinazoendelea, ni kusaidia maendeleo endelevu katika sekta binafsi kwa nchi zinazoendelea na kwa njia hii kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

**SANDUKU 2: WASHIRIKA WENGINE NA WAFADHILI**

KPL inashirikiana na mashirika makubwa kama vile kampuni ya mbegu na madawa ya kilimo SYNGENTA ya Uswisi na kampuni kubwa ya kimataifa, Yara, ya mbolea ya Norway. Syngenta na Yara zinafanya kazi pamoja kwa kishirikiana na KPL ili kuimarisha thamani ya mchele na ushirikishwaji wa wakulima wadogo Kilombero35. Ushirikiano unahusisha uanzishwaji wa aina mpya ya mpunga, na uendelezaji wa matumizi ya mbolea ya Yara36. Syngenta imeipatia KPL mashine ya kusafisha mbegu37. Aidha, Yara imechukua jukumu kubwa katika kuendeleza dhana ya Ukanda wa Ukuzaji Kilimo (Agricultural Growth Corridor) katika mpango wa SAGCOT38 na ilifanya moja ya uwekezaji mkubwa wa kwanza chini ya SAGCOT kupitia ujenzi wa kituo cha mbolea kilicho gharimu dolla za kimarekani milioni 20 katika bandari ya Dar es Salaam39.

KPL inapata pia msaada mkubwa wa kifedha na vitendo kutoka katika taasisi mbalimbali za kimaendeleo. Misaada ya Kituo cha Mafunzo na Huduma za Usimamizi Afrika UNDP (ATMS) kwa KPL inahusisha idadi ya mikataba ya usimamizi40, ikiwa ni pamoja na kuazimwa wafanyakazi wawili wa KPL-Meneja Uzalishaji wa Mazao anayewajibika na usafishaji wa shamba, uzalishaji wa mazao, ufugaji, na uvunaji; na Meneja wa mitambo ya kukoboa mpunga atakaye wajibika na usimamizi wakati na baada ya mavuno41.

Mwaka 2013, Justine Greening wa DfID alitangaza dolla milion 10 za kimarekani kama mkopo kwa KPL ilikusaidia kufadhili mpango wa wakulima wadogo na mtambo wa kukobolea mpunga kwa madhumuni ya umwagiliaji. Wakati wa tangazo, Greening alisema, "kuwajibika katika uwekezeji unatoa fursa na matarajio ya kiuchumi kwa jamii. Ni busara kwetu kufanya kazi na wafanya biashara ili kuhakikisha mipango yao inasaidia jamii"42. Msaada wa DfID katika shirika unachukuliwa kama usio nufaisha wawekezaji wa kilimo wa AgDevCo, ambao ni maalumu katika kutambua, kuendeleza, na kupanga hatua za mapema kifedha kwa ajili ya fursa za kilimo endelevu na kilimo cha usindikaji biashara Africa43. AgDevCo inafadhiliwa na wafadhiri wengine miongoni mwao wengine ni mfuko wa Rockefeller, USAID, Muungano wa Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), Kurungezi Kuu ya Ushirikiano wa Kimataifa wa wizara ya mambo ya nje ya Kiholanzi (DGIS) na DfID44. Mwakilishi kutoka AgDevCo pia ni mjumbe wa bodi ya wazazi ya kampuni ya KPL Agrica (angalia Kiambatisho 2)45. KPL inapokea pia msaada wa ziada kwa ajili ya mpango wake wa ukuzaji kutoka Mfuko wa Changamoto za Biashara African (AECF) na USAID. Maelezo zaidi juu ya hii yametolewa katika sehemu ya mfano wa ukuzaji wa KPL.

Serikali ya Norway kupitia bajeti ya maendeleo, imetenga pesa kwa ajili ya mfuko wa uwekezaji wa Norfund, mfuko umewekeza dolla za kimarekani milioni 10 katika hisa za kampuni ya Agrica[31]. Kampuni zote za Norfund na Capricon zina wawakilishi kwenye bodi ya Agrica (Angalia kiambatisho 2)[32].

AAC ni mfuko wa uwekezaji wa kilimo cha biashara, unasimamiwa na washirika wakuu wa Mauritius. Ulianzishwa kwa muungano Mfuko wa Gatsby Charitable, Mfuko wa Rockefeller, Mfuko wa Bill na Melinda Gates, na benki ya uwekezaji ya J.P. Morgan kufadhili yenye uwezo mkubwa barani Afrika. Miongoni mwao wamefanya ufadhili wa dolla milioni 25 za uwekezaji katika mfuko huo. Wakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID) ilitoa mikopo ya asilimia 50 kudhamini mfuko wa uwekezaji wa J.P Morgan[33]. Washirika wakuu wanadai kwamba uwekezaji wa AAC katika shirika la Agrica AAC ulikuwa muhimu katika kuchochea mradi, kuwezesha kampuni kununua shamba na kuvutia uwekezaji wa ziada ya dolla za kimarekani 25 milioni[34]. Ukubwa wa uwekezaji wa AAC ndani ya Agrica haujulikani. Mwaka 2008, KPL ilikamilisha upatikanaji wa hekta 5818 za shamba linalojulikana kama shamba la Mngeta.

Shamba hili awali lilianzishwa mwaka 1986 kama mradi kati ya rais wa kwanza wa Tanzania Julius K. Nyerere na Kim Il Sung kupitia ushirikiano wa serikali ya Tanzania na Korea Kaskazini (KOTACO). KOTACO ilitafiti shamba, ikalipa fidia, ikajenga km 185 za barabara na takriban km 290 ya mitaro ya maji, na kuanza kuzalisha mpunga kwa takribani hekta 2,500. Baada ya kuwekeza zaidi ya dolla za kimarekani milioni 25 katika mradi ambao haukuisha, mwaka

## KIELELEZO 1: MUUNDO WA UMILIKI WA SHIRIKA LA KPL[49]




1993 KOTACO ilifirisiwa ikiacha shamba na mitambo yake katika shirika la RUBADA[47]. Mwaka 1999, shamba la Mngeta lilifanya mkataba na kampuni ya Kilombero (KIHOCO). KIHOCO kamwe haikuweza kuanzisha uzalishaji katika zaidi ya hekta 400, na baada ya kushindwa kulipa kodi kwa miaka mitano, iliondolewa katika shamba Agosti 2007. Hii ilitoa fursa kwa shirika la Agrica. Shirika la umma na binafsi la KPL lilipata shamba la Mngeta kutoka kwa RUBADA kwa dolla za kimarekani milioni 2.55 Septemba 2008, ikilipa asilimia 50 za fedha taslimu na kubadili kiasi kilichobaki kuwa asilimia 8.3 ya hisa za KPL. Pamoja na uwekezaji unaotarajiwa kutoka shirika la Agrica, milki za shirika la RUBADA zinatakiwa kupunguzwa kwa asilimia tano au pungufu yake[48].

Baada ya kukamilka kwa upatikanaji wa ardhi, KPL ilianza shughuli za kuendeleza shamba la Mngeta. Kwa kuanzisha teknolojia ya kilimo cha chini , lengo lililoelezwa ni kupunguza gharama kwa mzalishaji swa ndani wa mpunga katika mazingira endelevu[50] . Agrica inadai kwamba mtazamo wake juu ya mstari wa faida ya watu na safari vilevile usikivu inaoonesha katika kuhakikisha matokeo yenye maendeleo makubwa na kutoa razini ya marejesho ya matarajio katika makundi ya wawekezaji wake mali na miradi uwekezaji katika kilimo[51]. Kufikia mwaka 2011, kampuni alikuwa imewekeza zaidi ya dalla milioni 30.5 za Kimarekani katika mradi wa KPL ili kumalizia na kusawazisha ardhi yenye 4229; usawazishaji wa hekta 3000, upatikanaji wa matrekta, mashine za kupandia na kuvunia; ujenzi wa ghala lenye mita za mraba 6,200, kinu cha kukobolea mpunga tani sita kwa saa, mashine yenye uwezo kujiendesha katika kusafisha na kukausha kwa urahisi tani 2,000, nyumba, ofisi, na karakana; kufunga mitambo ya umwagiliaji katika eneo la hekta 215; na uzinduzi wa mpango wa shamba dogo (zaidi ilijadiliwa katika kifungu cha mlolongo wa thamani ya ushirikiano).[52]

Katika msimu wa tatu wa upandaji wa KPL (2011), shamba lilizalisha takribani tani 13,500 za mpunga (mpunga ambao haujakobolewa) kutoka hekta 4178, na akawa mzalishaji mkubwa pekee wa mchele53 Afrika Mashariki. Uzalishaji kamili mwaka 2017, inatarajiwa kwamba shamba litazalisha tani 53,000 za mpunga, ambayo kwa mujibu wa kampuni itaongeza uzalishaji wa kitaifa kwa asilimia 4.5[54]. KPL imeendeleza biashara yake ya jumla ya mpunga inayojulikana kama "Mama mchele" (Bi Rice) na huuza zaidi katika -uzalishaji wake katika shamba lango kwa zaidi wanunuzi 180 wa moja kwa moja kutoka ndani ya Tanzania[55]. Katika mkoa Dar es Salaam, KPL huuza kwa wanunuzi wa moja kwa moja kutoka katika ghala lake na kupitia tume ya uhalifu wa masoko ya nafaka ya jumla[56]. kwa mujibu wa nyaraka za kampuni, KPL pia inapanga kutafuta fursa kwa ajili ya mauzo kwa nchi jirani[57].

Mwezi Julai 2010, kampuni mama ya KPL , Agrica, ilipewa hadhi na mkakati wa mwekezaji na serikali ya Tanzania. Mkakati huu wenye ruzuku ikiwamo kusamehewa kodi kwenye misamahara na ushuru wa mafuta na vifaa vya nje, ikiwa ni pamoja majani ya mimea na mfumo wa kilimo cha umwagiliaji katika Agrica[58]. Mwaka 2011, kampuni alieleza nia yake ya kuwa karibu zaidi na uwekezaji ili kupata ziada ya hekta 5,200 za ardhi, km 20 kutoka Mngeta kwa ajili

**KISANDUKU NA 3: BONDE LA KILOMBERO**

Shamba la Mngeta liko katika sehemu ya kusini mashariki ya Bonde la Kilombero, mkoani Morogoro, kuhusu 450 km kutoka Dar es Salaam. Kilimo ni kuongoza shughuli za kiuchumi katika eneo hilo pamoja na mpunga, mahindi, mihogo, na kunde kama mazao msingi kwa familia za wakulima. Ufugaji pia ni mkubwa. mkoa wa Morogoro ni kawaida inajulikana kama moja ya "vikapu chakula" katika Tanzania na rutuba yake juu inafanya eneo la uwezo mkubwa wa kilimo. Kwa sababu hii, eneo ni walengwa kama kipaumbele marudio kwa ajili ya uwekezaji chini ya SAGCOT, hasa kwa ajili ya uzalishaji wa mchele na sugarcane.[62]



Mwonekano wa Bonde la Kilombero. © Greenpeace




ya upanuzi wa baadaye wa KPL ili kuboresha uongozi, vifaa, na uwezo wa usindikaji.[59] Hata hivyo, katika barua pepe ya mwaka 2015, Mkurugenzi Mtendaji wa Agrica, Mheshimiwa Coleman, anadai kwamba KPL haina mipango tena ya kupanua zaidi shamba lake la Mngeta, kwa sababu zilizodhaniwa kuwa ni changamoto za mazingira ya kibiashara.[60]

Kipindi cha mpito kutoka zama za KOTACO mpaka KPL mwaka 2008 iliruhusu vijiji vinavyozunguka eneo hilo huingia katika mazingira kwa kupanua matumizi ya ardhi yao kupitia makazi, ufugaji na kilimo katika ardhi isiyotumika. Hii imesababisha "mgogoro wa kufukuzwa" katika eneo walilofikia KPL.[61] Kuna vijiji vitatu vinavyopakana na mashamba makubwa ya KPL-Mngeta, Mkangawalo na Lukolongo-ambayo vimeathiriwa na maendeleo mapya ya kilimo

## Kutengeneza Nafasi kwa Ajili ya Kiini cha Shamba: Kunyang'anywa Ardhi na Makazi Mapya.

Mgogoro wa kufukuzwa wakulima unaohusishwa na mwendelezo wa shamba la Mngeta ulianza kutokana na agizo la serikali la mwaka 2008 lililoagiza wanakijiji wanaoishi au kulima ndani ya eneo linalojumuisha takriban asilimia 25 ya mashamba kuacha ardhi. Wakati baadhi wakitii amri ya kufukuzwa, wanakijiji wengi waligoma wakidai kuwa walikuwa watumiaji halali wa ardhi.

Katika kukabiliana na mgogoro uliojitokeza, KPL ilikamilisha tafiti mbalimbali kwa lengo la kuelewa vizuri kuendelea kwa mienendo ya uvamizi wa baadhi ya maeneo ya mashamba '. Hizi ni pamoja na

miongoni mwa mambo mengine, Ripoti ya utafiti wa vibarua wa shamba la Mngeta .[63] Ripoti hiyo, ambayo ilikamilishwa mapema mwaka 2009, imebaini kuwa hali ilikuwa ngumu na nyeti kijamii kwa idadi kubwa ya watu kuishi na au kulima ndani ya eneo la mashamba lililopendekezwa.[64] Hivyo, kusafisha uchafu na kufyeka mashamba kwa ajili ya kilimo na KPL itasababisha makazi yao ya kiuchumi kuwa na athari mbaya kwa maisha yao.[65] Mnamo Oktoba 2009, shamba lilitembelewa na Waziri Mkuu wa Tanzania kama sehemu ya dhamira yake ya kukuza mpango wa Kilimo Kwanza ambapo KPL baadaye ikawa mradi wa maonesho. Wakati alipozuru shamba, Waziri Mkuu anadaiwa kuelekeza mamlaka za wilaya kutatua suala la wanakijiji kuzuia shughuli za kilimo, ingawa aliwataka kufanya hivyo kwa njia sahihi na kujiepusha na matumizi ya nguvu katika mchakato huo.[6]

## Mpango wa Makazi Mapya Hatua

Kutokana na hali hii, KPL ilijiingiza katika mchakato wa kuondoa wanakijiji kupitia Mpango wa Utekelezaji (RAP), kutoka eneo la mradi kwa kuandaa makazi mapya. RAP, ilifuata miongozo ya Benki ya Dunia katika kuandaa makazi mapya yasiyo ya hiari (Viwango vya Utendaji Na. 5 juu ya Jamii na mazingira endelevu IFC), ilielezwa kuwa vijiji viwili katika vitatu vilivyopo karibu na mashamba makubwa, Mngeta na Lukolongo, kaya 230 zilikuwa moja kwa moja zimeathiriwa na mapendekezo ya shughuli za KPL.[67] Kwa mujibu wa RAP, kaya hizi, zilitumia eneo linalojumuisha robo moja ya shamba la Mngeta ambalo lilikuwa na idadi ya watu 1,258.[68] RAP ilisema kuwa kaya zilizoathirika zingeweza kukabiliwa na moja au mwingiliano wa yafuatayo: upungufu wa nyumba; hasara ya mashamba; hasara ya upatikanaji wa maji; hasara ya kipato na uhakika wa maisha; na hasara ya mazao.[69]

Katika kusimamia athari hizi hasi, lengo kuu la RAP, kama ilivyoelezwa na KPL, lilikuwa ni:

"... Kuwa na mpango wa makubaliano kwa ajili ya makazi ya watu ambao wataathiriwa na utekelezaji wa mradi. Aidha, mpango utaweka wazi namna utakavyokabiliana na changamoto za kuhamia makazi mapya, na masuala ya fidia yanayohusiana na utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha maisha ya Watu Walioathiriwa na Mradi(PAPs) yanaboreshwa au yanarejeshwa kama yalivyokuwa awali kabla ya mwanzo wa utekelezaji wa mradi. "[70]

RAP alipendekeza hatua mbalimbali za kuchukuliwa ili kupunguza athari juu ya kaya zilizoathirika, bila kujali uhalaliwa umiliki wao. Hizi ni pamoja na malipo ya fidia kwa hasara ya mazao na nyumba; ujenzi wa maeneo mapya ya makazi na nyua; na utoaji wa maeneo mashamba mbadala .[71] Aidha, RAP ilitanabaisha kwamba " umakini utazingatiwa katika kufikia mwafaka mzuri na mtu mmoja mmoja kwa kaya zilizoathirika bila kumlazimisha mtu yoyote kuingia katika makubaliano ya jumla asiyoridhika nayo."[72]. RAP inaendana vema na miongozo ya Benki ya Dunia ya miundo ya makazi na ya kiuchumi kuhusiana na ununuzi kwa kiasi kikubwa cha ardhi: miongozo inaeleza kwamba pale ambapo zoezi la uhamishaji wa makazi ya watu "haliwezi kuepukika," uhamishaji wa makazi hayo sharti uzingatie kurejesha au kuboresha maisha ya watu walioathirika .[73]

Baadhi ya wadau wanaona kuwa uhamaji huu usio wa hiari kupitia miongozo hiyo, umeandaliwa kama fursa kwa ajili ya kuboresha maisha na maendeleo kwa wakazi wanaopokonywa ardhi yao.[74] Katika hatua nyingine zaidi miongozo inalichukulia suala la umilikaji wa ardhi kwa kiwango kikubwa kwa wafanyabiashara wakulima kama nyenzo ya msingi katika kuyafikia maendeleo ya kilimo. Hivyo, suala la kuwaondoa wakulima wadogo linaweza kuwa ni jambo lisiloepukika lakini utoaji wa gharama kwa ajili ya maendeleo yao ni suala muhimu. Hoja ya msingi hapa ni kwamba watu walioathirika wanalitazamaje suala hili kama fursa kwa ajili ya maendeleo yao.

## Makazi Mapya na Utekelezaji wa Fidia: Mchakato wenye Ubishani na Msuguano

RAP inakadiria kuwa kaya 80 kati ya 230 kaya zilizoathirika, hukabiliwa na upungufu wa nyumba pamoja na ardhi, ambapo zizobaki 150 hukabiliwa na upungufu ardhi ya kulima pekee.[81] Hata hivyo kaya hizo zote huhesabiwa kuwa zinastahili kupewa fidia na KPL.

Nchini Tanzania, sheria ya ardhi inahitaji malipo ya fidia kamili, ya haki, na haraka kwa mtu yeyote ambaye anamiliki ardhi kwa haki, aliyetambuliwa kuitumia ardhi kwa muda mrefu, au kubatilishwa kwa matumizi ya kimila ya ardhi.[82] Fidia lazima izingatie zoezi la tathmini, ambalo linapaswa kuzingatia thamani ya mali katika soko, gharama za kujikimu, posho ya usumbufu, posho usafiri, na gharama ya kupata ardhi mbadala.[83] Ingawa sheria inatoa mianya ya kinga kuhusiana na fidia, kwa kuwa Tanzania hakuna sheria mahususi zinazosimamia mchakato

**KISANDUKU NA. 4: JUKUMU LA USHIRIKI KWA JAMII: KPL NA MAENDELEO YA JAMII**

Kama sehemu ya mkataba wake wa kukodisha ardhi na kuelekea kwenye uwajibikaji kwa kijamii, KPL aliahidi kuvipatia vijiji vitatu vinavyolizunguka shamba shilingi milioni 50 ($ 29,000) za mfuko wa maendeleo ya jamii.[75] Fedha hizo hugawanywa kwa vijiji hivyo kwa kulingana na idadi ya watu katika kila kijiji, kwa lengo la kusaidia miradi ya maendeleo inayopangwa na wanavijiji wenyewe. Jukumu la KPL ni kuhakikisha kuwa fedha zinatumika vizuri, na kusambaza vifaa vya ujenzi kwa ajili ya miradi ya jamii badala ya kuchangia fedha, na kusimamia ujenzi kupitia idara ya majengo ya shamba.[76] utoaji wa fedha za maendeleo umejigeza kwenye "uhusiano wa ujirani mwema" kati ya KPL na wanakijiji.[77] vijiji Jirani wanatarajiwa kushirikiana na KPL kwa kufanya "kila wanaloliweza katika kulinda shamba kutokana na wezi, Wavamizi na Waharibifu." Kama vijiji watashindwa kutimiza majukumu yao kama majirani wema, sehemu ya mfuko inaweza isitolewe. [79] Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Agrica, Mheshimiwa Coleman, mfuko huo hadi sasa umeichangia shule mpya (madarasa mawili) na makazii ya mwalimu katika kijiji kimojawapo, kituo kipya cha afya, na miradi ya maji safi katika vijiji vyote vitatu.[80]



Nyumba 2 katika 1 zilizojengwa kwa ajili ya walimu katika shule ya msingi Mbasa. © Oakland Institute



Madarasa 2 yaliyojengwa katika shule ya msingi Mbasa. © Oakland Institute



Mwonekano wa ndani ya darasa katika Mbasa shule ya msingi. © Oakland Institute



Pampu ya maji ya kusukuma iliyojengwa katika shule ya msingi Mbasa. © Oakland Institute

unaohusiana na makazi mapya. Hivyo, kama Mthamanishaji mmoja wa serikali alivyonukuliwa akisema: "... katika matukio kama haya mengi huwa ni juu ya watu wenyewe kujitafutia maeneo mapya." [84] Hata hivyo, kwa upande wa KPL, kwa kuzingatia mchakato wa uthamanishaji unaondamana na kanuni hapo juu , kaya zilizoathirika watapokea malipo ya fedha na / au aina stahiki ya fidia.[85] Fidia zisizohusisha pesa taslimu ni vitu kama vile ardhi, nyumba, vifaa vya ujenzi, na / au mikopo ya kifedha. [86]

makazi mapya na mchakato wa fidia uliofanywa na

KPL[87] umepongezwa sana na aghalabu umechukuliwa na kuonekana kama mfano wa kuigwa na wawekezaji wengine katika eneo la kilimo.[88] Uchambuzi uliofanywa na Bill na Melinda Gates Foundation unadai kuwa mchakato wa makazi mapya umeboresha viwango vya maisha ya watu waliothiriwa na mradi.[89] utafiti huo anasema kuwa mojawapo ya mafanikio ya KPL ni kuaminika na kujenga uhusiano mzuri na jamii.[90]

The Oakland Institute imefanya mahojiano na wanakijiji katika jamii zinazoizunguka kati ya mwaka 2011 na 2015, hata hivyo, inaonyesha kwamba uwekezaji wa ardhi na mchakato wa fidia vimeendelea kuwa na ubishani na msuguano mkali: "mchakato mzima imekuwa kama wa kiimla" mwanakijiji mmoja alisema.[91]

Kweli, wanakijiji wanalalamika kwamba kuna kupishana kwingi kati michakato iliyoandaliwa ya KPL na hali halisi ya yale yaliyofanyika. Ebu tuanze kuchunguza wanakijiji 150 ambao walipokonywa mashamba baada ya kuendelezwa kwa KPL katika shamba la Mngeta. Wanakijiji hawa 150 walikuwa na uchaguzi wa aina kuu tatu: [92]

1. KPL kuwatafutia eneo jipya la ardhi linalofikia ekari tatu katika maeneo ya jirani,
2. Wangejitafutia wenyewe ardhi mbadala ambapo KPL ingetoa fidia ya kiwango cha juu cha Shilingi 30,000 ($ 17) kwa ekari, au
3. KPL ingefidia pesa taslimu kulingana na thamani ya soko.

Aidha, KPL ilijitolea kusaidia shughuli za maandalizi ya shamba kwa mwaka wa kwanza kwa ardhi mpya.[93] Hata hivyo, wanakijiji kadhaa wametutaarifu kwamba baada ya ardhi yao kuchukuliwa na KPL, walilazimishwa kukubali fidia, ambayo iliwawezesha kupata ardh ndogo ukilinganisha na kiasi cha ardhi walichomiliki awali. Mwanakijiji mmoja alieleza:

> "Wao wakaniuliza 'unataka tukupatie pesa ununue ardhi wewe mwenyewe, au unataka sisi kukupa eneo jipya la ardhi?" Ndipo wakaniambia kwamba ikiwa ninataka kununua ardhi mpya mwenyewe, thamani kwa eneo la ekari tatu itakuwa shilingi 90.000 ($ 49,77). Kwa hiyo niliona ni salama zaidi kulipwa fidia kwa ardhi mpya ya ekari tatu, ingawa mwanzoni nilikuwa na shamba la ekari 11."[94]

Wanakijiji wengine ambao walichagua kupewa fidia ya pesa taslimu wamelalamika kwamba kiasi cha fedha walichopewa hakina uwiano na thamani ya ardhi yao katika eneo hilo. RAP imeeleza kuwa "kwa upande wa mradi wa shamba la Mngeta uthamanishaji ulisimilisha shilingi 30,000 ($ 17) kwa ekari kulingana na bei ya sasa ya soko la Mkangawalo" (moja ya vijiji vya karibu) ikichukuliwa kama rejea kwa ajili ya fidia kwa malipo ya ardhi.[95] Hata hivyo, wanakijiji walieleza kuwa fidia iliyolikuwa inayotolewa ilikuwa ni shilingi 10,000 tu ($ 6) kwa ekari, pasipo kupokea maelezo yoyote yanayofafanua ni vigezo vipi kampuni imetumia kuwapatia kiasi hicho.

Haieleweki ni kwa nini wanakijiji wamepewa theluthi moja tu ya thamani inayohitajiwa kutoka kwa RAP. ujibu wa Carter Coleman, jumla ya shilingi 10,000 ($ 6) kwa ekari zililipwa kama fidia kwa madai ya ardhi kame kwa eneo lisilolimwa linalozidi ekari 3. Hata kama kiasi kamili cha shilingi 30,000 ($ 17) kama fidia , ni dhahiri kwamba uthamanishaji wa ardhi kwa ajili ya fidia ulikuwa wa chini sana. Kwa bei ya soko la Tanzania mwaka 2014 kiasi hicho kinawiana na kilo 25 za mchele.[96] Fidia iliyotolewa pia ilikuwa chini sana ikilinganishwa na bei ya kukodisha ardhi katika maeneo ya jirani ilikuwa haitoshi hata kukodisha sehemu kwa ajili ya msimu mmoja: Mwanakijiji alieleza kwamba "kabla ya KPL kuja hapa ilikuwa inawezekana kukodisha ardhi kwa shilingi 20,000 ($ 11) au 30,000 ($ 17) kwa ekari kwa mwaka, lakini kwa sasa, unahitaji kulipa shilingi 100,000 ($ 55) kwa ekari . Kwangu mimi, gharama hizo ni kubwa, hivyo itakuwa sio rahisi kwangu kufanya hili tena."[97]

Ardhi inayofaa kwa kilimo Marekani inanunuliwa kwa $ 6,000 hadi $ 11,674 kwa ekari, zaidi ya $ 2,000 kwa Brazil na $ 400 hadi $ 600 nchini Zambia.[98] Unapolinganisha na kile wanachokilipa wawekezaji ili kupata ardhi inayozalisha katika maeneo mengine duniani, kiasi kilichotolewa kwa wanakijiji ambao wamepoteza ardhi yao kwa ajili ya mradi huu inaibua maswali mazito kuhusu mradi kwa madai ya kujinadi kuwa azma yao ni kuleta maendeleo na kwa kutoa fidia ya haki kwa watu walio ondolewa katika makazi yao.

Maendeleo ya mradi yameleta madhara ya mfumuko wa bei katika soko la eneo husika, ambayo imefanya

kuwa vigumu sana kwa wenyeji kukodi ardhi ya kilimo kwa sasa. Kama ukizingatia kwamba KPL imechukua eneo lote lenye ardhi nzuri, na hivyo kuzuia matumizi ya baadaye ya ardhi kwa wakulima wadogo wadogo wa Tanzania, hata hivyo masuala ya fidia yenyewe yanaleta mashaka. Wanakijiji walioteseka kutokana na kunyang'anywa ardhi wamekabiliwa na gharama kubwa pale walipojaribu kuanzisha makazi mapya. Mahojiano na wananchi juu ya suala hili inaonyesha hali kuwa mbaya zaidi kwa baadhi ya kaya hasa katika suala la kipato na usalama wa chakula.

"Kwa kuwa nilikuwa na ekari 5 nilipewa shilingi 50,000 ($ 27.65) kama fidia. Pia nilipata fidia kwa ajili ya miti yangu ilyokuwa katika shamba, lakini ilikuwa haitoshi. Nina familia ninayoitunzaji, hivyo sio jambo zuri. Nilijisikia vibaya sana kwa ajili yao. "

-mwanakijiji, Novemba 201499

Aidha, RAP ilisisitiza katika mikutano mbalimbali kwamba kulikuwa na maeneo ya kutosha ya ardhi katika vijiji vya jirani kwa ajili ya kukidhi uanzishwaji wa makazi mapya.[100] Hata hivyo, hili lilikuwa tofauti kabisa na mtazamo wa jumla miongoni mwa wanakijiji kwa kuwa maeneo mazuri kwa kilimo nje na shamba la Mngeta yalikuwa machache sana, hali imekuwa mbaya sana[101] Mtazamo huu ulionekana ukiwasukuma wanakijiji wengi wakati wa mchakato wa fidia. Mhojiwa mmoja alisema:

> "Walitupatia namna za uchaguzi. Walisema kwamba kama wewe hutaki kupewa shilingi 10,000 ($ 6) kwa ekari, unaweza kupewa ardhi. Hata hivyo, tatizo ni kwamba ardhi waliyokuwa wakiigawa ilikuwa imejaa maji hivyo, watu wengi waliochagua ardhi badala ya kupewa pesa ni kama hawajafidiwa kabisa, kwa sababu ardhi hiyo haifai kwa kilimo cha aina yoyote. Wakati huo sikujua, ila nilichojua ni kwamba kuna uhaba wa ardhi nzuri hapa, hivyo nilikuwa nikifikiri, ni wapi ambako wangeweza kutupeleka? Kwa hili akilini, niliamua kuwa itakuwa salama kukubali malipo ya fedha taslimu."[102]

Baadhi ya wanakijiji hawakukubali uchaguzi wowote na waliambiwa na serikali ya kijiji kuwa kulikuwa na uhaba wa ardhi katika eneo hilo na kwamba ardhi iliyokuwapo tayari wamepewa KPL. Wanakijiji walielekezwa kukubali fidia ya fedha kwa ajili ya mali zao zilizopotea na walishauriwa kwenda kutafuta wao wenyewe maeneo mapya kwa ajili ya shughuli za kilimo.[103]

## Maeneo ya Makazi Mapya: Hayatimizi Ahadi za RAP

Kama sehemu ya mpango wa kuhamishwa kwa kaya 80, ambazo zilipoteza nyumba na ardhi ya kulima, KPL ilionyesha kuwa kungejengwa nyumba mpya za makazi na maeneo muhimu ya kijamii katika makazi mapya.[104] Moja ya maeneo haya liko ndani ya eneo lenye watu, 389 kwa ha za eneo, ambalo KPL waliamua kulimega kutoka shambani ili kupunguza haja ya kuanzisha makazi mapya ili kuokoa gharama (eneo liliopo ndani ya mpaka mwekundu katika kielelezo na. 2 hapo chini). Kaya ishirini zilikuwa zimehamishiwa kwenye nyumba mpya katika eneo jekundu, na kaya zilizobaki zilipelekwa kwenye nyumba mpya ndani ya mipaka ya kijani nje ya shamba. Nyumba mpya zenye vyumba viwili zilijengwa kwa matofali ya kuchomwa, zenye paa la mbao, sakafu ya saruji, kuta za matofali, zilizoezekwa kwa mabati, zenye choo cha nje, na vyumba vya jiko. Aidha, kaya hizi 80 zilitengewa ekari tatu za ardhi ili kuendeleza maisha yao.[105] Kwa mujibu wa RAP, makazi mapya yangewezesha watu walioondolewa kwenye makazi yao kuendeleza au hata kuboresha hali zao za maisha.[106]

MCHORO 2: SHAMMBA LA MNGETA NA MAKAZI MAPYA





Makazi mapya ya eneo la Mbasa © Mikael Bergius–The Oakland Institute

Hata hivyo, wanakijiji katika moja ya haya maeneo mapya ya makazi (Mbasa) walieleza kwa uwazi kutoridhika na hali ya makazi. Suala moja la msingi ni mahali lilipo eneo hilo, ambalo lilikatwa na KPL kwa makazi mapya katika shamba. Wakati wa msimu wa mvua, eneo hilo hukumbwa na mafuriko hivyo kuwa hatarishi kwa kuishi. Ingawa uongozi wa KPL unaonekana umekuwa ukilitambua suala hili kwa miaka kadhaa, kama ilivyokuwa Novemba 2014, walishindwa kukabiliana na suala hilo. Ushahidi wa picha za video uliopelekwa kwa The Oakland Institute zinaonyesha maji yakiwa yametuama katika nyumba mpya. Mmoja wa wanakijiji aliyehamishwa alisema

> "Wakati maji yanapoingia ndani ya nyumba huwa tunasimama usiku kucha bila kulala kwa sababu nyumba yote huwa imejaa maji. Mafuriko yanapofikia kiwango kibaya baadhi ya wanyama wetu hufa na huwa ni hatari kwa maisha yetu, na hasa watoto, wanapocheza. Lilikuwa janga."[107]

Ripoti ya uchunguzi wa hivi karibuni inaonyesha matukio kama hayo kutokea katika maeneo mengine ya makazi mapya yaliyojengwa na KPL.[108] Kwa miundo ya makazi, wanakijiji walionyesha kukerwa
na kampuni kwa kuwa kile kilichowasilishwa kwao kama ndoto za kufikia maendeleo ghafla ikageuka ukweli usiowavutia.

> "Walikuja na kuchukua ardhi yetu na nyumba, lakini waliahidi kutupatia nyumba mpya za kisasa ambazo tunaweza kuishi na familia zetu, na basi hiki ndicho walichotupatia. Hii si nyumba. KPL imetuletea tabu. "[109]

Nyumba hizo zina vyumba viwili (takriban 3.5m x 3.5m) vilivyotenganishwa kwa ukumbi mwembamba, nyumba hizo pia haziwiana na matarajio yaliyoletwa na KPL, na muhimu zaidi, ni kwa mahitaji ya kila siku ya wanakijiji. Ukilinganisha nyumba zao mpya na kile walichokuwa nacho kabla ya makazi mapya.

Wanakijiji wanadai kwamba ingawa majengo mapya yamejengwa kwa vifaa vya kisasa, nyumba zao za awali zilikuwa na uwezo wa "kubeba familia kubwa, ziliwafaa

na zilikidhi mahitaji yao, na zilikuwapo kwenye eneo bora zaidi."[110] Wahojiwa pia walionyesha kutoridhika na nyumba mpya.[111] Kumbuka kutoka mwanzo kwamba katika RAP waliahidi kuwa "watafanya maridhiano mazuri na mtu binafsi" na kwamba hakuna hata mmoja

"atakayelazimishwa akubali maamuzi ya jumla au ya wengi ambayo haridhiki nayo.." [112] kwa kuwa wamejazana pamoja katika eneo dogo "kama kambi" - na hujiuliza kwa nini KPL hawakujenga nyumba mpya katika maeneo kwa kufuata matakwa binafsi. Kampuni hiyo pia ilieleza katika RAP kwamba kaya za makao



Mafuriko katika eneo la makazi ya Mbasa, Machi 2014 (picha na wanakijiji)

mapya na kaya zilizopo ndani ya maeneo teule ya makazi zitapewa hati ili kumiliki ardhi ya mahali wanapoishi kisheria.[113] Hata hivyo, kwa mujibu wa waliohojiwa, kwa mfano mahojiano ya Novemba 2014, hakuna mwanakijiji yeyote aliyepokea hati ya umiliki au kuwa na ushahidi wowote wa umiliki wa nyumba mpya.[114] Hivyo, inaonekana muhimu kuuliza kama wanakijiji hawa wamepokea fidia yoyote ukuzingatia hawana uwezo wa kuwa wamiliki wa moja kwa moja wa nyumba mpya au kuwa na haki ya umiliki wa ardhi ambayo nyumba zimejengwa. Akijibu hili, Mheshimiwa Coleman, kwa mawasilianoya barua pepe na The Oakland Institute, alidai kuwa ardhi na nyumba zipo chini ya umiliki wa wanakijiji wenyewe.[115] suala hili bado ni kizungumkuti na linahitaji uchunguzi zaidi.

Hali kadhalika, siyo kaya zote zilizoathirika kwa nyumba na ardhi yao walipewa nafasi ya kuwa na uchaguzi wa njia mbadala, kama alivyoahidiwa kwenye RAP. mwanakijiji mmoja alieleza kuwa yeye alikuwa na taarifa kwamba jamaa yake alikuwa miongoni mwa wale ambao ilibidi kupewa nyumba kati ya zile zilizotengwa kwa makazi mbadala. Ingawa, hadi Novemba 2014, hakuna nyumba mpya iliyokuwa imetolewa kwa familia hiyo. Alieleza:

> "Mimi sikupewa nyumba mpya ya kukaa. Walipofika hapa, waliniambia kwamba kama nitatoa ardhi kwa KPL wangeweza kunijengea nyumba mpya na kunipatia fidia yangu kulingana na kiasi cha ardhi niliyowapa. Lakini hawakufanya hiyo, wao walitutupa nje na kutupatia fedha kidogo za kutuwezesha kuishi."[116]

Kaya hii ililazimika kutumia gharama kubwa ili kupata makazi mapyakwa kuwa tangu watolewe nje ya eneo la shamba la Mngeta walilazimika kupanga nyumba. Hili limekuwa gumu sana katika kuchukulia na yale yalipo kwenye RAP, ambayo inasema waziwazi kwamba nyumba mpya zitajengwa katika hatua za awali ili kuhakikisha kwamba watu walioathirika "hawatatoa gharama yoyote kuhusiana na kukodisha nyumba au mahitaji kwa ajili ya malazi." [117]

Wakati ingali haieleweki ni kwa jinsi gani wanakijiji wengi wameathiriwa na hali hii, utafiti unaonyesha kwamba hili halikuwa suala pekee lenye vuguvugu.[118] Aidha, wanakijiji wengi tangu wahamishwe hadi sasa hawajapata sehemu mbadala za kulima, kama alivyoahidiwa na KPL, na hili lina madhara kuhusu usalama wa chakula.[119] Mwaka 2010, wanakijiji waliipelekea barua kampuni ya KPL kuwakumbusha jukumu lao la kikamilisha fidia kwa watu walioathirika na mradi.[120] Ahadi hii ilitimizwa baadaye, baada ya miaka mitano. Aidha, baadhi ya wale ambao walipewa ardhi mbadala walilalamika kwamba ardhi mpya ilikuwa haifai, na haiwezekani, kwa sababu eneo hilo linatuamisha maji wakati mwingi.[121] Baadhi ya wanakijiji walilazimika kukodi ardhi nyingine ili kuendeleza maisha yao, wakati wengine ambao hawakuweza kumudu malipo ya kukodisha mashamba walilazimika kuwa vibarua wa ujira mdogo.[122] Mwanakijiji mmoja alieleza:

> "Maisha sasa ni magumu sana ukilinganisha na awali. Hapo mwanzo nilikuwa na uwezo wa

kupata fedha kutoka kwenye shamba langu mwenyewe, lakini sasa ninapata fedha kwa kufanya kazi ndogo ndogo. Hivyo maisha siku hizi ni tofauti sana, hayana uhakika. Kwa mfano, awali nilikuwa na uwezo wa kulima chakula changu mwenyewe, lakini sasa nahitajika kununua chakula kwa hicho kipato kidogo ninachokipata."[123]

## Ukosefu wa Taarifa na Uwazi

Baadhi ya wanakijiji wamedadisi kuhusu ukosefu wa taarifa na uwazi wakati wa mchakato wa fidia. Wanadai kwamba KPL kwa mambo mengi imekuwa ikihusiana na serikali ya kijiji, na taarifa chache ndizo wamekuwa wakipelekewa wanakijiji wenyewe. Kwa mfano, wahojiwa walieleza kuwa"hawakushirikishwa kuhusu kiasi gani cha fidia kimeamuliwa, na kwamba walipewa tu taarifa kwamba wanatakiwa kupokea fedha hizo na kama wewe hutaki hicho kilichotolewa unaweza kuacha," hakukuwa na maelezo yoyote kuhusu jinsi mali yao ilivyothaminishwa.[124] Suala la ukosefu wa taarifa limesababisha kuchanganyikiwa na kutoaminiana miongoni mwa wanakijiji, ambao wanaitupia mashtaka KPL kwa kutathmini mashamba ya wanakijiji kiholela na kutoa fidia ndogo mno ikilinganishwa na thamani ya kila shamba. Walihisi kudharauliwa kwa kiasi kidogo cha fidia iliyotolewa, mhojiwa mmoja alisema: "sikuweza kuchukua fedha; ni afadhali kufa maskini kuliko kuchukua hiyo fedha. "[125]

Kwa baadhi ya wanakijiji ilikuwa vigumu kufikiwa na kiasi cha fidia wanayostahili. Wanakijiji walioathirika walitakiwa kupokea fidia kutoka kwa KPL ama kwa njia ya benki au kwa utaratibu wa malipo ya fedha taslimu, ambao ulitakiwa kufanywa rasmi mbele ya Kijiji na maafisa wa Kata.[126] Katika mahojiano, wanakijiji walieleza kuwa KPL badala yake ililipa fidia kupitia serikali ya kijiji, ambayo kwa kwa namna moja ina wajibu wa kuwalipa wanakijiji. Mwanakijiji mmoja alisema, "Mimi sijui chochote; nimepewa fedha kutoka mfukoni mwa kiongozi wa kijiji."[127] Utaratibu huo usioeleweka umesababisha matatizo na kuchakachuliwa kwa mchakato mzima wa fidia. Mwanakijiji huyo aliendelea:

"Walipomaliza hesabu ya mashamba yetu, hatukuambiwa ni kwa njia gani na lini fidia yetu tutaipata. Tulipowaona baadhi ya majirani zetu wakipewa fidia zao tukafanya ufuatiliaji na



Mashine ya Hassam ya kukoboa mpunga Mngeta. © Greenpeace

serikali ya kijiji ndipo tukapewa shilingi 120,000 ($ 66). Tukarudi kwa serikali yetu ya kijiji na tukauliza kwa nini tumepewa kiasi hiki kidogo kwa eneo kubwa la ardhi tulilokuwa nalo. Lakini hatukupewa majibu yoyote. Baada ya kufanya ufuatiliaji wa mara kadhaa, kiongozi wa kijiji hatimaye alitupatia shilingi nyingine 300,000 ($ 166) moja kwa moja kutoka mfukoni mwake. Tangu siku hiyo tukaondolewa kutoka kwenye ardhi yetu mpaka sasa, hii ndiyo fidia pekee tuliyoipata na ilichukua miezi tisa. Na tuliahidiwa kupewa nyumba mpya kwa kuwa nyumba zetu za zamani zilibomolewa, lakini hatujapewa nyumba yoyote. Badala yake kwa sasa tunaishi kwenye nyumba za kupangisha."[128]

Wanakijiji walionyesha kuwa kinyume kutokana na maoni yao ya uwepo wa mradi, ambao awali ulielezwa kwao kuwa ni fursa kwa maendeleo, maendeleo ambayo hawakuyafikia kwa kushindwa kuitumia ardhi vyema. Mwanakijiji mmoja aliongea kwa lugha ya msisitizo kuelezea uzoefu wake kuhusiana na mradi:

"Hapo awali, watu walikuwa na mashamba yao na nyumba zao wenyewe na waliweza kuishi kwa kushirikiana na heshimiana. Sasa, wengi wa hawa hawana ardhi au nyumba zao tena. Kwangu mimi, KPL imetuletea taabu. Ni kama wamenichimbia shimo, na kunirushia ndani yake. Hawajatuletea maendeleo yoyote, ni hasara tupu. Baada ya KPL kuwasili, maisha yangu yamekuwa jehanamu. Kila siku, hali zetu zinaendelea kuwa mbaya zaidi. "[129]

## Muunganiko wa Kimkufu- Thamani: Kuvuna Zaidi ya Mchele?

Mwaka 2009 KPL ilianzisha mpango mdogo kusaidia uzalishaji wa mpunga katika mashamba yao. Mtaalam kutoka India alianzisha SRI kwa mashamba ya mfano, na kuwapa mafunzo wafanyakazi wa KPL na familia 15 za majaribio kwa kulima katika teknolojia ya SRI (Box 4) .[130] Mwaka 2011, kwa msaada wa kifedha kutoka Norfund, KPL ilipanua mpango hadi kufikia familia 265.[131] Mwezi Mei 2011, KPL alipata tuzo ya African

KISANDUKU NA. 5: MFUMO WA KUONGEZA UZALISHAJI WA MCHELE

Mfumo wa kuongeza uzalishaji wa mchele (SRI) uliasisiwa na kutumiwa Madagascar miaka ya 1980 kama kiungo muhimu cha kimfumo kwa mafunzo ambapo ilisababisha mavuno ya kushangaza na kupunguza kwa kiasi kikubwa cha uingizaji wa nje. Mfumo umejigeza katika upandikizaji wa peke yake, kuacha nafasi pana, kutumia miche mIdogo, kupunguza viwango vya umwagiliaji (mazoezi ya mbadala wa unyevu-na-kavu), mara kwa mara kupalilia na jembe la kuzunguka, na matumizi ya mbolea zisizo za viwandani. Kutokana na kuweka nafasi kubwa kati ya mbegu, msongamano wa mimea katika mfumo SRI huwa mdogo kuliko kama ilivyo katika upandaji wa kawaida. Hii inapunguza ushindani kati ya mimea na inaruhusu mfumo wa mizizi kuzama kwa kina kirefu ambayo husaidia kuongeza matumizi ya virutubisho vya udongo na maji kwa ufanisi zaidi Licha ya kupungua kwa msongamano wa mimea, msongamano wa mashina yanayozalisha hukadiriwa kuwa mkubwa zaidi kuliko katika mifumo ya kawaida na kusababisha kuongezeka kwa mavuno na uzalishaji majani. Kwa jumla, zifuatazo ni kanuni za SRI:



Mazao ya SRI © Mikael Bergius—Oakland Institute

- Kupanda mapema, haraka na ili kupata mimea yenye afya;
- kupanda kwa kuacha nafasi katika mistari ya miraba husababisha kupungua kwa msongamano mimea;
- Kuboresha matunzo ya udongo kwakuusawazisha, kurutubisha kwa mbolea ya viumbe hai na kupalilia; na,
- Kupunguza matumizi ya maji kwa kuweka vipindi (unyevu na kavu).

Kwa SRI siyo lazima kutumia mbinu za  pembejeo zitokanazo na viumbe hai katika kilimo. Kwa KPL, mbinu zote hutumika ikiwa ni pamoja na matumizi ya pembejeo za viwandani.[133]

Enterprise Challenge Fund (AECF) ruzuku ya $ 750,000 ili kuongeza program za SRI.[132]

AECF ilianzishwa kama mkakati wa ushirikiano maalum katika kuunga mpango wa Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA). AGRA hutoa msaada wa utawala na vifaa na ni chombo halali katika kukamilisha malengo kupitia AECF, wakati huohuo usimamizi wa kazi wa siku hadi siku hufanywa na KPMG International Development Advisory Services.[134] Kupitia ruzuku ya AECF, KPL ilipanua mpango wake wa washirika wadogo hadi kufikia wakulima 1,350 mwaka 2012 na waliongeza wakulima 3,225 katika mwaka 2013.[135] Programu hiyo pia hupokea msaada kutoka USAID kwa ajili ya mpango wa baadaye, ambao hugharamia mafunzo na mishahara ya maafisa ugani, pamoja na mafunzo kwa wakulima.[136]

Kwa mujibu wa KPL, mpango wa SRI ulikuwa umetoa mafunzo kwa jumla ya wakulima 6,527 katika mbinu mpya za kilimo kwa mwaka 2014.[137] KPL ilieleza kuwa kuanzishwa kwa SRI kumechangia kuwainua wakulima wadogo kutoka kilimo cha kujikimu hadi kilimo cha kupata ziada, na wakulima waliripoti kupata maradufu au hata mara tatu ya mavuno yao kutoka tani moja hadi mbili kwa hekta hadi nne na tani sita kwa hekta.[138] Maafisa ugani wa KPL waliunda makundi 25 ya wakulima[139] ili kufanya " mashamba darasa".[140] Mara baada ya mafunzo, kila mkulima hupewa mfuko wa mbegu bora na mbolea za viwandani na kujitoa kulima 1/4 ya ekari moja ya ardhi yao wenyewe kwa kutumia mbinu za SRI. Mafunzo kupitia SRI hutolewa kwa mbinu zilizo rahisi na kanuni ya msingi inayotumika katika SRI ni kupanda kwa kuacha nafasi kwa mistari ya mraba.[141]

Baada ya mwaka mmoja wa mafunzo, wakulima huwa wanastahili kuwa wazalishaji bora kwa KPL na hupokea mikopo ya uzalishaji.[142] mikopo hutolewa na taasisi ndogo ndogo za fedha (MFI) kama vile National Microfinance Bank (NMB) na

Youth Self Empryoment Foundation (YOSEFO) .[143] KPL pia ilishirikiana na Kampuni ya mbolea ya Yara Norway, kwa ajili ya usambazaji wa mbolea ya viwandani kama sehemu ya kuongeza uzalishaji wa mkopo .[144] Kama ilivyokuwa mwaka 2014, wakulima 800 (nje ya 6,527 waiopata mafunzo) walishirikiana na KPL na kupokea mikopo ya uzalishaji ya mradi wa wakulima wadogo .[145] kwa mujibu wa KPL, mradi ulihitajika wakulima wadogo kati ya 2,500 na 5,000 ili kujiendesha kibiashara.[146]

## Mkataba wa Wakulima Wadogo

Mradi wa wakulima wadogo umeunganishwa na uhusiano wa kimikopo, ambapo taratibu za makubaliano na mkataba umewekwa kati ya KPL na wakulima. Ambapo wakulima wadogo huendelea kutumia ardhi yao, wanakubaliana kupitia mkataba juu ya nini kizalishwe, jinsi ya kuzalisha, nini cha kufanya baada ya mavuno, na bei wanaletewa."Kama wewe ulichukua mkopo ni wajibu wako kukubali zana zinazotolewa na KPL. Hata kama huzitaki, au hauziitaji, lazima kukubali ili upate mkopo, "mkulima mmoja alisema.[147] Wakulima pamoja na maafisa ugani wa SRI wanahoji kuhusu matumizi ya mbolea za viwandani katika eneo ambalo lina udongo wenye rutuba nzuri.[148]

Sampuli ya mkataba wa mwaka 2012/2013 katika msimu wa kilimo ulikuwa na masharti yafuatayo:

- Wakulima wadogo watapewa mkopo wa shilingi 400,000 ($ 220).
- Wakulima wadogo watatumia mkopo huu katika uzalishaji wa mchele tu kupitia shughuli SRI.
- Kutoka kiasi hiki cha pesa, wakulima wadogo lazima wanunue pembejeo za shilingi 194,000 ($ 105).
- Pembejeo hizo zinajumuisha kilo 12 za Saro 5 za mchele (TZS 24,000- $ 13); mbolea ya viwandani ikiwa ni pamoja na Yara Mila nafaka kilo 50 (TZS 50,000- $ 27) mbolea ya basal na Yara Urea kilo 50 (TZS 50,000- $ 27) kwa ajili kukuzia na vifaa vya kupalilia (TZS 70,000- $ 38).
- Wakulima wadogo watalipa sehemu ya mkopo kwa fedha taslimu kabla ya mavuno (tazama hapo chini) wakati deni lililobaki watalipia mpunga.
- Mpunga lazima ufikie viwango vilivyoelezwa na ulinunuliwa (2013) kwa bei ya shilingi 6,000 ($ 3) kwa debe (takriban kilo 20).
- Bei iliyopangwa haibadiliki, pasipo kujali bei iliyopo sokoni.

Wakulima wengi ambao waliingia katika utaratibu wa ripoti ya wakulima wadogo walifanya shughuli zao kwa matarajio makubwa. Kwa jumla, walifurahia mafunzo waliyopata, walishuhudia mbinu mpya za kilimo zilivyochangia mavuno bora. Kwa kweli,wakulima wadogo wameonekana kuvuka malengo katika mashamba ya KPL kwa uzalishaji bora kwa hekta.[149] Wakulima wadogo waliotazamiwa walishawishiwa kwamba kujiunga na mradi ingekuwa fursa nzuri ya kuboresha maisha yao kwa kupitia ongezeko la uzalishaji, usalama wa soko, na vipato vya


Mchele ukiwa unauzwa sokoni. © Greenpeace

juu. Mwanakijiji alitaarifu kwamba, "Nilidhani kwamba kwa kupata mkopo, pamoja na maarifa mapya juu ya SRI, hali yangu ingeboreshwa kwa kiasi kikubwa." [150]Hata hivyo, kile kilichoonekana kuwa fursa na faida kubwa mara kimegeuka na kuwa mzigo wa madeni makubwa kwa wakulima wadogo wengi.

## Mizigo ya Madeni

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, sehemu ya mkopo ilibidi kulipwa kabla ya mavuno. Ndani ya wiki mbili za kupokea mkopo wa awali wa shilingi 400,000 ($ 220), jumla ya awamu kumi za kwanza za shilingi 15,000 ($ 8) kwa miezi mitano mfululizo zilipaswa zilipwe.[151] Gharama hii ilikuwa ngumu kumudu kutoka kwa wakulima wadogo walio wengi ambao aghalabu walikosa fedha za kukabiliana na gharama nyingi za mwanzoni mwa msimu wa kilimo. Washiriki wengi walikabiliwa na wasiwasi mara kwa mara ndani ya kaya zao kama wangekuwa na uwezo wa kulipa mikopo kwa wakati.

Wakati wakulima wadogo wamesaini mikataba, waliambiwa kwamba bei kwa ajili ya ulipaji wa mpunga haibadiliki kwa kulingana na thamani ya soko la mpunga kwa wakati huo. Hata hivyo kilipofikia kipindi cha uvunaji wakulima walilalamika kwamba bei halisi waliyopokea kutoka KPL ilikuwa ya chini.

Sababu moja ya mabadiliko hayo inaonekana kuwa ni mabadiliko katika sera ya bei ya nchi. Ili kulinda wazalishaji wa ndani wa mchele, Jumuiya ya Afrika Mashariki ina viwango vinavyolingana vya Ushuru wa nje (CET) wa asilimia 75 ya mchele unaoingizwa kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2013, serikali ya Tanzania ilisamehewa tani 130,000 za mchele kutoka CET.[152] Serikali ilidai kuwa licha ya kujitosheleza katika mchele, Tanzania ililazimishwa kuendelea kuingiza mchele kutokana na uhaba wa mchele wa kisasa uliosababishwa na uhodhi wa wafanyabiashara wa mchele.[153] Hata hivyo, msamaha wa ushuru ulisababisha kuanguka kiasi kikubwa kwa bei ya jumla kwa asilimia 54 ilipofika Juni 2013.[154] KPL inadai kwamba licha ya anguko hili katika bei ( bei ya mpunga vijijini ilidaiwa kuwa shilingi 4,000 ($ 2.16) kwa debe (kilo 20) , na katika uzingatiaji wa ahadi za kimkataba, bado wazalishaji walilipwa shilingi 6,000 ($ 3.24) kwa debe.[155] Hata hivyo, wakulima walieleza kwamba walitakiwa kulipa bei kulingana na kubadilika kwa hali ya soko. Kama mmoja wa wakulima wadogo wa zamani alivyosema:

> "Ghafla waliongeza debe la ziada la mchele kwa kile tulichotakiwa kulipa hapo awali. Ingawa mikataba ilisema kuwa walitakiwa kununua mchele kutoka kwetu kwa shilingi 6,000 ($ 3.24) kwa debe, wao walinunua kwa TZS 3,000 tu ($ 1.62). Walituambia tu ni kuwa hali ya soko ilikuwa imebadilika. "[156]

Hali tete ya soko ambayo kwa sehemu imechangiwa na sera ya serikali, inaaminika kuwa imeleta changamoto kubwa kwa wote KPL na wakulima wadogo wadogo wa mchele. Hata hivyo, kimahusiano ya wakulima wadogo, washirika wadogo wako katika hatari zaidi kwa kuwa wao ndio wanalazimika kubeba sehemu kubwa ya hasara kwa kuuza mchele kwa bei ya chini ya soko. Hii inakiuka mipango ya mikataba. Suala hili linaibua swali kuwa bei iliyowekwa katika mkataba wa wakulima wadogo haibadiliki tu kwa wenye uwezo mdogo. Hili linaonyesha tatizo la kimahusiano kiutawala katika mradi kwa kupuuza kuutekeleza mkataba uliowekwa awali. Kama mmoja wa wakulima wadogo alivyosema wakati wa kujadiliana kuhusu marekebisho ya bei na KPL: "Hilo lilipotokea, nikagundua kwamba watu hawa wananinyonya tu na wanatumia kigezo cha kwamba sisi ni duni na wao wana uwezo." [157]

Punguzo la bei lililotolewa na KPL lilizidisha tatizo la madeni kwa wakulima wadogo wengi na kuendelea kutenda kazi kwa kinyongo. Pamoja na kwamba wakulima wengi walikuwa na uwezo wa kuongeza uzalishaji kwa mbinu mpya, walieleza kuwa kipato chao kinaishia kwenye kulipia madeni.
Kwa mujibu wa mkulima:

> "Mimi nilikuwa nakaribia kumaliza deni langu kwa KPL, lakini nilipolipia kila kitu sikubaki na mchele wala pesa yoyote. Mchele niliotunza kwa chakula nikawa nalipia deni. Kwa hiyo, ili kupata pesa ya kuwalisha wanangu nililazimika kuuza vitu vidogo vidogo vya ndani nilivyokuwa navyo"[158]

Pasipo kutarajia wakulima wengine waliuza mali zao walizozitegemea sana na mifugo yao ya thamani ili kulipia madeni na wengine walishindwa kurejesha. Kwa mujibu wa nyaraka za kampuni, mojawapo wa MFI’s (taasisi ndogo ya kifedha) ilikuwa ikitoza karibia kiasi cha asilimia 50 kwa walioshindwa kurejesha mikopo kwa wakati mwaka 2013.[159] Katika kesi hizi, wanakijiji walielezea, MFI huwafikia wadaiwa ili warejeshe mikopo yao. Mwanakijiji alieleza:



Mwanamke anang’oa magugu karibu na shamba la KPL. © Greenpeace

> "Kama mtu hana uwezo wa kulipa madeni yake, kisha KPL hutoa taarifa kwa MFI. Kisha wao [MFI] kumfilisi kwa mdaiwa kwa kuchukua mali zake, kama vile kitanda, baiskeli, na godoro, au kitu chochote cha thamani. Watu wengi hapa wamekumbwa na madhila haya. Baadhi ya watu hata wamelazimika kuuza nyumba zao."[160]

Kwa mujibu wa mahojiano, matarajio na ndoto walizokuwa nazo wakulima za kuwa na maisha bora siku za usoni hazikutimia. Wakati huohuo tathmini ya jumla ilionesha kuwa kupitia mpango wa mafunzo kwa wakulima wa SRI uliboresha na kuongeza mavuno kwa wakulima,[161] waliohojiwa wanakubaliana kuwa mpango wa wakulima wadogo ni kama ndoto za usiku. Aghalabu, waliohojiwa walidai kuwa baada ya kushiriki kwa mwaka katika mpango huo, wakulima wengi wadogo hawakuwa na hamu ya kushiriki tena. Hii ni kati ya sababu zilizofanya pasiwepo na wakulima wanaopatiwa mikopo katika msimu wa kilimo wa sasa (2014/2015).[162] Mmoja wa wakulima wa awali alieleza uzoefu wake kuhusu KPL:

> "Nilipogundua kuwa kushiriki katika mradi huu kunaniongezea gharama kuliko faida, niliamua kuacha. Kwa kweli, niliwapa zaidi ya kile nilichovuna. Ni bora zaidi kufanya kazi wewe mwenyewe kuliko kufanya kazi kwa wezi. Hivyo ndivyo walivyo."[163]

Akielezea kwa hisia kama hizo, mwanakijiji mwingine akasema:

> "Kabla sijaingia katika mradi huu wa wakulima wadogo, maisha yangu hayakuwa rahisi sana, lakini yalikuwa mazuri. Baada ya kujiunga na mradi huo, hali yangu ikawa ngumu sana. Ilikuwa ni usumbufu kufikiri kuhusu mkopo na kuhusu kutokuwa na uwezo wa kupata mavuno ya kutosha. Nilikosa uhuru. "[164]

Madai kuwa wakulima wanatumia maarifa mapya ya SRI kuboresha uzalishaji badala yake, wamegundua njia mbadala za kupata huduma za mikopo na masoko ya mazao yao. Aidha, baadhi ya waliohojiwa walipendekeza kwamba muundo wa makubaliano ambayo wakulima waliingia KPL inaelekea kuunufaisha upande mmoja ambao kwa mujibu wa mkataba gharama zilizotumika lazima zirudi wakati upande wa pili unaweza kupoteza. Kwa kawaida, wakulima hawa wana vyanzo zaidi ya kimoja vya kuingiza mapato nje ya kilimo katika miradi, ambayo husaidia kuondokana na vikwazo kuhusiana na



Mfanyakazi wa KPL. © Greenpeace

malipo ya madeni kama ilivyoelezwa hapo juu. Hili, kwa kiasi fulani, linaleta mkanganyiko wa kiuchunguzi kuhusu KPL na inaashiria kwamba utafiti zaidi kuhusu mienendo ya usawa katika mazingira ya ndani unahitajika. [165]

## Uhuru Hatarishi wa Wakulima

Mwisho, uhusiano wa ukiritimba kati ya KPL na wakulima inaonyesha hatari kwa wakulima kujisalimisha uhuru wao kuhusu nini na jinsi ya kuzalisha na wapi kwa kuuza bidhaa zao. Vipengele vingi vya uzalishaji vimejikita kwenye mkazo wa ulipaji madeni unaodhibitiwa na kampuni, hivyo kuwapa wakulima nafasi kidogo kwa ajili ya majaribio. Haipingiki, kwa mkulima kukabiliana na hali ya majaribio ambayo ndio malengo mawili katika mpango wa SRI.[166] KPL ya SRI, hata hivyo, inadaiwa kuwa ni "mpango wa kutumika, badala ya kuwa kuchukuliwa, na wakulima wadogo." [167]

Mtindo huu unaweza kumwondoa mkulima kutoka kwenye kilimo cha kuzingatia mbinu za uzalishaji na kuelekea kilimo kinachosimamiwa na maslahi ya kilimo cha biashara, [168] kama ilivyosisitizwa na KPL wakishirikiana na Yara kuhusu usambazaji wa mbolea za viwandani. Mabadiliko haya yamehatarisha na kudhoofisha uhuru wa wakulima na kuwabadilisha kutoka kuwa mkulima na kuwa vibarua katika nchi yao wenyewe bila kuwa na maamuzi yoyote ya nini wakifanye.[169] Tishio hili liliwapata wengi wa wakulima wa awali katika KPL ambao walihojiwa katika utafiti huu. Mmoja wao akasema:

> "Kupitia mkataba, sisi tulilazimishwa kukubali teknolojia ambayo kimsingi hatukuihitaji ili kupata mavuno mazuri. Maamuzi yote kuhusu kilimo yalifanywa na KPL. Kwamba unapaswa kufanya hivi na unapaswa kufanya jinsi wao wanavyotaka. Kwa kuwa nilikuwa na deni nilifanya kwa kadri wanavyotaka. Sikuwa huru,

> kwa sababu una shamba lako mwenyewe na kila kitu, lakini unaamriwa na mtu mwingine. Kwa sababu ya hili, nimeapa kwa nafsi yangu kwamba kamwe siwezi kufanya biashara tena na KPL."[170]

Hata hivyo, kukiwa hakuna wakulima waliopokea mikopo ya uzalishaji kwa msimu huu wa kilimo (2014/2015), KPL sasa inafanya kazi na wawekezaji na benki za ndani kuanzisha upya mradi wa wakulima wadogo. Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji Agrica, Mheshimiwa Coleman, KPL ina matumaini ya kuhusisha wakulima wengi wa SRI waliopokea mafunzo, na KPL kupitia mkataba wa ununuzi wa mpunga msimu wa kilimo wa 2015/2016.[171]

## Ajira

Uwezo wa kuzalisha fursa mpya za ajira na usababishaji wa njia mbalimbali za mapato vijijini aghalabu inanukuliwa kuwa utatokana na uanzishwaji wa mashamba makubwa.[172]

Mapema KPL ilivyokutana na vijiji vya jirani vya shamba la Mngeta, fursa mpya za ajira lilichukuliwa kama moja ya mambo makubwa mazuri yanayoletwa na athari za uwekezaji. Kwa mujibu wa KPL, kampuni iliajiri takriban watu 270 wa ajira ya kudumu Mei 2015.[173] Katika mahojiano na gazeti moja la Tanzania, Mkurugenzi Mtendaji wa Agrica, Mheshimiwa Coleman, alinukuliwa akisema kuwa "uanzishwaji wa ulipwaji wa mishahara kwa fedha taslimu umebadilisha hali ya eneo linalolizunguka shamba la KPL [174]

Wafanyakazi wa kudumu ni pamoja na wahasibu, walinzi, makatibu, madereva, waendeshaji wa harvester, wakoboaji wa mpunga, na wasimamizi, wakati kazi za muda hufanywa na vibarua wa kupalilia na kuvuna mpunga. Kiwango cha chini cha mshahara kilichowekwa katika kilimo Tanzania ni shilingi 3,846 ($ 2.2) kwa siku na shilingi 100,000 kwa mwezi ($ 58).[175] KPL inadai kulipa asilimia 20 na asilimia tano zaidi katika mshahara wa chini kwa wafanyakazi wa kudumu na vibarua mtawalia.[176] Hata hivyo, kulipa juu kidogo ya kiwango cha chini cha mishahara haina maana kwamba mshahara wanaopewa wafanyakazi unawatosheleza na wa haki. Mhojiwa mmoja ambaye alikuwa akifanya kazi kama mlinzi alilalamika kuhusu mshahara chini: "Niliacha kazi kwa sababu mshahara haukuweza kusaidia familia yangu. Ninalinda mali za kampuni zenye thamani ya mamilioni ya dola na halafu angalia ninachokipata. "[177]

Ushahidi katika kumbukumbu za wafanyakazi, unathibitisha, kuwa KPL ilipunja mishahara ya baadhi ya wafanyakazi wake wa kawaida. Katika matukio kadhaa, waliohojiwa walisema mishahara kwa wafanyakazi wa kawaida huanzia kati ya shilingi 2,000 ($ 1) na TZS 3,500 ($ 2) kwa siku. Hata hivyo, wanakijiji huendelea kutafuta ajira katika mashamba ili waweze kutatua shida zao ndogo ndogo kwa mapato ya fedha taslimu. Mfanyakazi mmoja mwajiriwa wa zamani katika jitihada za kutibu ndugu yake wa familia alisema:

> "Ujira mdogo nilioupata katika shamba haukuniwezesha kuwa na kipato cha kutosheleza mahitaji yangu na hususani kushindwa kumlipia matibabu ndugu yangu mgonjwa. Lakini niliendelea na kazi kwa sababu bado nilikuwa nahitaji fedha kwa wakati huo, na naweza kufanya hivyo tena kama kuna hitaji. Hata hivyo KPL inafaidi kutokana na umaskini uliopo katika vijiji vya hapa. Tunatumikishwa kupita kiasi, na wao hufaidika kwa kutumia wafanyakazi wao maskini."[178]

Pamoja na mishahara midogo, vibarua pia walielezea juu ya ukosefu wa vifaa muhimu vya kinga kazi kama vile buti, ovaroli, glovu, na kofia. Baadhi ya wafanyakazi walilalamika kuhusu kutokwa vipele kwenye ngozi na mwili kuwashwa na hakukuwa na upatikanaji wa matibabu kutokana na kukabiliwa na aina mbalimbali za hatari katika shamba (kwa mfano kuumwa na nyoka) na madhara madawa ya kemikali.[179] Aidha, kuna kuchanganyikiwa miongoni mwa wanakijiji kwamba KPL inatoa upendeleo kwa watu wa nje badala ya watu wa ndani kwa upande wa kazi za kudumu.[180] Kutokana na hali hii, ni vigumu kuona ni jinsi gani fursa mpya za ajira zinaweza kuleta mabadiliko kwa wanajamii.

## Masuala ya Mazingira

Mashamba ya KPL yameanzishwa katika Bonde la Kilombero, yenye eneo la $km^2$ 7,967, ambalo linachukua wastani wa asilimia 20 katika Bonde lote la Kilombero. Uwanda wa bonde hilo umesheheni ikolojia na bayoanuai za thamani na lina jumuisha mito mingi sana, ambayo inasababisha maji safi ya msimu katika uwanda wa chini Africa Mashariki.[181] Eneo ambalo shamba la KPL limo, limejumuishwa katika RAMSAR ambayo ni makubaliano ya kimataifa kuhusu maeneo owevu muhimu (tazama sanduku 3). Kilimo cha uzalishaji wa mashamba makubwa katika eneo hili ni tishio kubwa kwa mazingira na viumbe hai vya asili hasa kutokana na ongezeko la matumizi ya madawa mbalimbali ya kilimo yenye kemikali.[183]

Ili kuongeza uzalishaji, KPL ina mpango ya kuunganisha mto ulio karibu na Mngeta ili kuwa na mifumo mikubwa ya umwagiliaji kwa gharama inatarajiwa ya $ milioni 25.[184] Januari 2011, kampuni ilianza majaribio ya kilimo umwagiliaji wa mchele katika hekta 215, ambayo imeonekana kuwa na mafanikio na inatarajia kukamilisha ujenzi na ufungaji wa mfumo wa nishati ya maji ya umwagiliaji unaojiendesha ifikapo 2017.[185] Kwa mujibu wa tathmini ya hivi karibuni ya Mazingira na athari za jamii (ESIA), KPL imepanga kutumia kilimo cha umwagiliaji misimu yote miwili: wa mvua na kiangazi ili kuzalisha mara tatu kwa mwaka.[186] KPL ina vibali kutoka Bodi ya maji ya Bonde la Rufiji[187] kuchepusha hadi asilimia 50 ya Mto Mngeta katika msimu wa kiangazi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ambao ungeweza, kuruhusu umwagiliaji wa hekta 3,000 huku mtiririko wa mto ukiendelea kuwa ndani ya viwango vinavyotakiwa.[188]

Mgawanyo huu upo katika mgongano ulio wazi na Mikakati hasa katika mto Mngeta, wataalamu wa umwagiliaji ya Tathimini za Athari za Kimazingira na Kijamii kwa mpango wa SAGCOT, ambao unapendekeza kwamba maendeleo yote ya kilimo cha umwagiliaji katika bonde la Kilombero yasitishwe hadi pale kutakapokuwa na maelewano mazuri kati ya upatikanaji na mahitaji ya maji kutokana na mafuriko mabaya kwa viumbe hai na watumiaji wa mito. Zaidi ya hapo, inaonya kwamba kukosekana uangalifu miongni mwake na upatikanaje wa data juu ya mtiririko wa maji katika bonde lenye mfumo wa maji, mavuno yanayochukua muda muda mrefu yameshuka, hasa majira ya kiangazi.[189] Kama ilivyo wanadai kwamba tayari umeathirika na mabadiliko ya hali ya hewa (tabia nchi).[190] Umwgiliaji wa KPL dhidi ya ESIA unathibitisha miongoni mwa shughuli kadhaa, miongoni mwa shughuli hizi, lakini inahitimisha kwamba madhara makubwa yasiyozuilika katika mpango kilimo cha umwagiliaji yanaweza kuzuilika ikiwa kutakuwa na usimamizi wa karibu na uongozi mzuri kwa kutumia njia mbalimbali. Hata hivyo, mipango ya umwagiliaji ya KPL kwa haraka inahitaji utafiti huru ili kuchunguza madhara ya muda mrefu na ya muda mfupi haya yanaweza kuwa katika uhusiano wa viumbe hai juu ya mafuriko na watumiaji wa mito.

Hii inahusika hasa katikamazingra ya SAGCOT ambapo mashamba kadhaa ya kibiashara ya umwagiliaji yamepangwa na yana umuhimu katika kukusanya mapato yake.[191]

Utengenezaji wa miundo mipya ya umwagiliaji umeripotiwa kutikisa ongezeko la migogoro katika ya KPL na vijiji vilivyo karibu na mashamba. Kazi ya utengenezaji inahitaji kuvunja moja ya barabara zinazokatisha shambani, ambayo inaunganisha vijiji viwili ambayo kwa upande mwingine inawalazimisha wanakijiji kuzunguka wanaposafiri kati ya vijiji



Sehemu ya Mkataba wa eneo owevu la Ramsar © Greenpeace



Mto Mngeta © Greenpeace

husika. Baadhi ya wanakijiji wanaitikia katika hili kwa kuchimba mtaro katika barabara kuu iendayo katika mashamba ya KPL ili kuzuia magari ya KPL kufika na kutoka shambani.[192] zaidi ya hayo, baadhi ya wanakijiji wamekamatwa wakifanya jaribio la kutaka kuchoma baadhi ya mashine za KPL zinazotumika katika ujenzi.[193] Bwana Coleman amedai kwamba mkutano wa hadhara ulioitishwa na wanakijiji umesaidia kutuliza ghasia.[194] Wanakijiji waliohojiwa, ingawa walikuwa na mitazamo tofauti na wanaarifu kwamba mgogoro wa barabara bado upo hata baada ya mkutano wa hadhara.[195]

Vilevile kuna wasiwasi mkubwa katika matumizi ya muda mrefu ya mbolea za viwandani zenye sumu na dawa za kuulia wadudu na sumu ya majani inaeza ikatokea kuwepo katika maeneo yao ya maji na udongo.[196] Wasiwasi huu unaongezeka hasa katika kipindi cha masika wakati ambapo kemikali zinaweza kutiririshwa katika mito na mikondo jirani na mazingira ya unyevunyevu, ambayo yanatumiwa na wazawa kwa malengo mbalimbali ya kimaisha. Katika shamba, KPL imetumia mchanganyiko mkubwa wa kemikali ilikuzuia wadudu waharibifu na magugu, ikijumuisha dawa maarufu ya kuuwa magugu zenye mkusanyiko wa Monsanto.[197] Kampuni inadai kwamba inafuata taratibu nzuri za kupunguza matumizi ya madawa ya kilimo yenye kemikali kwenye mashamba na itazuia matumizi ya dawa hizo wakati wa masika.[198] Haijawekwa wazi ni vipi mipango ya umwagiliaji inaathiri matumizi ya dawa za kemikali za kilimo.

Hata hivyo, jamii zinazozunguka shamba zinadai kuwa na uzoefu wa madhara yanayotokana na matumizi ya kemikali za kilimo kutoka kwa KPL kutokana kuchimbuka na kuondoshwa kwa ardhi.[199] Kwa mujibu wa wanakijiji, matumizi ya kemikali za kilimo kwa ndege yameathiri mazao ya wakulima jirani na kukuza wasiwasi wa kiafya yanapochafua visima vya maji yanayotumika kwa kunywa na matumizi mengine ya nyumbani.[200]

Mwaka 2010, zaidi ya wakulima 600 wa vijiji jirani kwa ujumla wao waliandika barua wakilalamikia kupoteza mazao yao na magonjwa kufuatia unyunyiziaji wa kemikali za kilimo wa anga. KPL imesimia Taasisi ya Uchunguzi wa Viuatilifu vya Kitropiki (TPRI) Arusha kuchunguza tatizo. TPRI imegundua kwamba mikondo ya glyphosate imekaa katika mashamba jirani ya mpunga, mahindi na mboga na kusababisha mazao kufa. Matokeo yake,Desemba 2011, wakulima 518 walifidiwa kwa madhara yaliyofanywa katika mashamba yao.[201]



Umwagiliaji wa mazao katika shamba la mpunga Agrica. © Greenpeace

Hata hivyo, wanakijiji wengi wanadai kwamba wengi walioathirika hawakupata fidia ambayo walistahili kupata. Katika mahojiano mkulima wa mahindi alisema:

> "Kemikali kutoka KPL zilitiririshwa hadi shambani mwangu na kuharibu mahindi yangu. Msimu huo sikuweza kuvuna chochote kwa sababu shamba lote liliharibiwa. Kwa hiyo nilisubiri mvua inyeshe ili iondowe kemikali zote ndipo nianze upya. Niligharamia gharama zote mimi mwenyewe, hivyo uchumi wa familia yetu uliyumba na ilisababisha upungufu wa chakula kwa mwaka huo."[202]

Kutokana na kujirudia kwa malalamiko, KPL kwa miaka ya hivi karibuni imerekebisha matumizi ya unyunyiziaji kwa kuanzisha kingo katika pembe za mashamba ili kuzuia kemikali za kilimo kutoka unyunyizia wa anga kutiririka katika mashamba jirani.[203] Bado baadhi ya wahojiwa wanalalamikia uharibifu wa mazao kutokana shughuli ya unyunyiziaji ya KPL.[204]

## Hitimisho

